TANGAZO LA SERIKALI Na. 210 la Tarehe 15/3/2019

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1)(q) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA ZA MWAKA, 2019

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa, Sheia Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Jiji la Tanga za Mwaka, 2019 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Tanga;

"Kitabu cha orodha" maana yake ni kitabu chenye orodha waliopokelewa na kulala katika nyumba ya kulala wageni husika;

"Mgeni" maana yake ni mtu yeyote anayepata huduma ya ma nyumba ya kulala wageni.

"Mmiliki" maana yake ni mtu ambaye anamiliki nyumba ya kulala inajumuisha msimamizi , mfanyakazi , wakala au meneja wa kulala wageni anayehusika na shughuli za usimamizi au nyumba ya kulala wageni;

"Nyumba ya kulala wageni" maana yake ni nyumba yoyote iliyojengwa kwa ajili ya matumizi ya biashara ya kulaza wageni kwa malipo;

"Stakabadhi" maana yake ni karatasi maalumu ya kuthibitisha malipo;

Ushuru wa nyumba za kulala wageni

4.-(1) Halmashauri itatoza Ushuru wa Nyumba za kulala Wageni kwa wamiliki wa nyumba za kulala wageni kwa kiwango cha asilimia kumi (10%) ya mauzo ya chumba au vyumba vya kulala wageni .

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa nyumba za kulala wageni baada ya mmiliki wa nyumba za kulala wageni kuwasilisha kitabu cha orodha kwa Afisa Mwidhiniwa kwa lengo la kukokotoa kiwango cha ushuru kinachopaswa kulipwa.

(3) Halmashauri inaweza ikakubaliana na Mmiliki au Wamiliki namna ya kulipa ushuru wa nyumba za kulala wageni.

Wajibu wa Halmashauri

5. Halmashauri itakuwa na wajibu wa:-

(a) kukagua nyumba ya kulala wageni kwa lengo la kutaka kujua kama wageni wote wameingizwa kwenye daftari la wageni;

(b) kukagua kama mmiliki au mtunza nyumba ya kulala wageni ana vitabu vya orodha ya kulala wageni vilivyoidhinishwa na Halmashauri;

(c) kukagua kama nyumba ya kulala wageni inafanya kazi lengwa na kama mapato ambayo hulipwa Halmashauri yanaendana na hali halisi ya mapokezi ya wageni;

(d) kukagua kama nyumba ya kulala wageni ipo katika hali ya usafi;

(e) kukagua kama kwenye Nyumba ya kulala wageni kuna mahitaji yote yanayo takiwa kuwepo kwenye nyumba ya kulala wageni;

(f) kukagua kama taratibu za kulaza wageni kwenye nyumba ya kulala wageni zinafuatwa.

Wajibu wa mmiliki

6. -(1) Itakuwa ni jukumu la kila Mmiliki wa nyumba ya kulala Wageni kuhakikisha kuwa:-

(a) analipa Ushuru wa Nyumba ya kulala Wageni kwa Halmashauri kila ifikapo tarehe 30 na si zaidi ya tarehe 05 ya mwezi unaofuata;
(b) ana kitabu cha orodha ya wageni na kukitumia kuorodhesha wageni wote wanaoingia na kulala kila siku;
(c) nyumba ya kulala wageni inakuwa safi muda wote;
(d) anatoa stakabadhi kwa mgeni baada ya kupokea malipo.

Taratibu za malipo ya wateja

7.-(1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atakuwa na wajibu wa kutoa stakabadhi halali ya malipo kwa kila mteja anayepata huduma ya malazi.

(2) Kila stakabadhi ya malipo inayotolewa ni lazima ionyeshe jina la mteja, tarehe ya kupata huduma ya malazi, kiasi cha malipo kilichotolewa na sahihi ya mpokeaji wa fedha hizo.

Makosa

8. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote endapo:-

(a) atashindwa kulipa ushuru ulioainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;
(b) atashindwa kuandaa na kutunza kumbukumbu sahihi kwa mujibu wa hizi;
(c) atamzuia afisa yeyote wa Halmashauri kusimamia utekelezaji wa hizi;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa lengo la kuficha au kukwepa kulipa ushuru.

Adhabu Kufifilisha Kosa

9. Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa la mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya hizi kwa kumtoza faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa ushuru anaodaiwa pamoja na faini.

---

**JEDWALI**

---

**HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA**
**(*Chini ya Kifungu cha 10)***

Mimi …………………………………………… (*jina la mtenda kosa*) ambaye ninaishi ……………………..(*mahali*) na kazi yangu ni………………………………, ninatambua na kukiri kuwa nimefanya kosa ………………………………………………. (*Aina ya kosa*) ikiwa ni kinyume na kifungu cha………………… cha za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Jiji la Tanga za Mwaka ,2019.

Kwahiyo, kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini: ……………………….......................
Mbele yangu:-
Jina: ……………………………………….
Saini: ……………………………………….
Wadhifa: …………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Jiji la Tanga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Tanga kilichofanyika Tarehe 30 mwezi Januari mwaka 2019 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikibandikwa mbele ya:-

**L.S**

……………………………………………………
DAUDI R. MAYEJI,
*Mkurugenzi wa Jiji*
*Halmashauri ya Jiji la Tanga*

……………………………………………………
SELEBOSS M. MUSTAFA,
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Jiji la Tanga*

NAKUBALI,

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais TAMISEMI*